

## COUNTY ASSEMBLY OF SAMBURU



### ***THE HANSARD***

**Thursday, 7<sup>th</sup> December 2023**

**The Assembly met at the County Assembly Chambers at 2:30 p.m.**

*The Speaker, (Mr. Lenamarle Stephen), in Chair*

### **PRAYER**

## **MOTION**

**Specially Elected MCA,** (Hon. Lenamatiyio Silapia): Thank you Hon. Speaker, I beg to move the following Motion:

**THAT**, pursuant to Standing Order No. 27 (4), this Assembly now adjourn for its long recess from today 7<sup>th</sup> December, 2023 until 13<sup>th</sup> February, 2024.

Thank you Hon. Speaker, I call upon Hon. Leerte to second the Motion

**MCA Poro Ward,** (Hon. Leerte Patrick): Mheshimiwa Spika naunga adjournmrnt kwasababu inawapatia Hon. Members kuweza kuwa na community katika Ward zao na pia kusherekea siku kuu ambazo ziko mbele zetu na kuweza kuangalia mambo zingine ambazo ziko katika Ward zao. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika naunga mkono, ahasanté.

**The Speaker,** (Mr. Lenamarle Stephen): I now propose the Motion, **THAT**, pursuant to Standing Order No. 27 (4), this Assembly now adjourn for its long recess from today 7<sup>th</sup> December, 2023 until 13<sup>th</sup> February, 2024. Hon. Silapia.

**Specially Elected MCA,** (Hon. Lenamatiyio Silapia): Thank you Hon. Speaker. I take this very important and great opportunity to thank God for enabling us to start they year since January up to today in good health and good progress as the County Assembly of Samburu. I think it is not a normal running of duty being cooperative since you joined us in this House. It is an opportunity that God enabled us and that is why we are adjourning today to go for a long recess which is a festive season also; there is Christmas, happy New Year.

I stand here to wish the Hon. Members a very protective and healthy Christmas and a happy new year and also pray for you that as we go for the recess, let us also remember to carry our duties at the ground and make sure that the Budget we approved in this House and all other things be implemented on the ground.

Hon. Speaker, let me take this opportunity to thank you for being a Speaker and an empire to this House without taking sides; you have really brought us together that we do all our things together without quarrelling since you joined this House.

I thank God, thank you, our clerks, our secretariat and everybody in the Assembly fraternity for the good unity since the beginning of this year, I think it is just not for granted but God has enabled us to be here today so that we can go for recess. I wish the Hon. Members a happy and protective recess during this festive season, I wish you a merry Christmas and a happy new year, thank you Hon. Speaker.

*(Applause)*

**MCA Ndoto Ward,** (Hon. Lealmusia Ali): Ahasante sana mstaahiki Spika. Nafurahi sana na nashukuru kwa fursa hii na nasema kwamba huu ni msimu wa siku kuu

*(Applause)*

na ni vizuri viongozi waende kujumuika na wenzao katika manyumbani pamoja na marafiki ili wapate sherehe ya kufana. Mstahiki Spika namshukuru mwenyezi mungu kwa kutuweka sisi kama jamii moja kwa muda wa mwaka moja sasa na najua kuwa tumejifunza mengi. Pia tumejaribu kuhudumia watu wetu kwa Nyanja mbali mbali kwa bidii na bila shaka natumai mwaka wetu umeenda kwa njia nzuri kwa sababu tumefanya maendeleo kadha wa kadha.

Tumetengeneza sheria ambalo ni jukumu letu kama viongozi. Kadhalika tumejaribu kukosoa ama kurekebisha mambo kadhaa kuhusu mambo ambayo wale wenzetu wapande ule mwingine wale wa serikali hii ya Kaunti inafanya na najua kwamba kuna miswada mbali mbali ambayo tumejadiliana mengine tumeyapitiza na mengine yako kwa njia na yanaenda kurekebishwa.

Namshukuru mwenyezi mungu pia kwa kutupatia wewe kama Mstahiki Spika wetu kwasababu tumekupata mwaka huu na umekuwa nasi takriban miezi saba ama nane hivi na tumefurahi kwamba tumekuwa pamoja na tumekuwa tukiendelea vyema mpaka sasa. Tunataraji mwaka ujao tutaenda kufanya bidi Zaidi ili tuweze kufanya jukumu zetu ambazo tunafaa kufanya.

Nawatakia wakilishi wa Wadi wenzangu sikuu njema na pia wale ambao tunafanya na wao hususan wale ambao wanaotusaidia katika Sheria na wale ambao wako na sisi kila wakati, nawatakia kila na heri na msheherekee vyema katika sikuu na Mungu atuweke salama hadi atakapotukutanisha tena.

Nasema asante kwa wote katika County Assembly, wafanyakazi na wale ambao walikuwa wakituhudumia kutoka nje kama wale wanaohakikisha kwamba tunapata maamkuli na pia wale

---

walio katika usafiri waliokuwa wakijitahidi sana, na najua mwaka ujao tutakapo kuja najua kwamba pengine itakuwa wakati wetu wa kuhamza katika jengo jipya; natumai tutafurahi kwani kuna nafasi kule na ofisi zetu zitakuwa.

Kwa hivyo hatutakuwa na wasiwasi ya kusanya watu hapa katika ofisi lako ama la Naibu Spika. Najua ofisi lilikuwa likifanya juhudzi sana kuhusu hayo. Kwa niaba yangu, ya Ndoto na familia yangu nawatachia kila la heri katika Maisha yenu, mungu awabariki na asante.

**Specially Elected MCA,** (Hon. Kagiri Stephen): Asante sana Mheshimiwa Spika. Namshukuru mwenyezi mungu kwa mwaka huu ambao tumekuwa hapa kama waheshimiwa. Nashukuru pia wafanyakazi wetu kwa kazi yao kwetu. Nashukuru Mweshimiwa Spika kwa muda ambayo umetuongoza. Najua sio mwaka mzima lakini tangu uingie ulijaribu kutuweka pamoja na nakushukuru. Nawatachia Krismasi njema na mwaka mpya njema ijayo, asante Mheshimiwa Spika.

**Specially Elected MCA,** (Hon. Mohammed Asha): Thank you Hon. Speaker. Nashukuru sana kwa muda huu ambao tumekuwa na wewe. Ninaunga mkono kuvunjwa kwa nyumba hili ili sisi kama wabunge tuweze kwenda kuwa na wenzetu, familia na wenzetu wengine. Mheshimiwa Spika unajua Kiswahili ni ngumu sana kigumu lakini ninajaribu Mheshimiwa Spika mimi ninapenda kusema nashukuru wabunge wenzangu na ningependa kusema wakati huu tunaenda kuwa na sherehe mbele yetu ya Krismasi mimi nawatachia Krismasi njema na mwaka mpya yenye mafanikio na Bwana Spika nakuomba wakati ambapo tutakaporudi mwenyezi mungu akitujalia tunaomba utuangalie sana. Bwana Spika tunashukuru umetushika hujatugawa katikati umetushika kama watu moja lakini tunaomba sana Bwana Spika wakati amabapo tutakaporudi tuangalie sisi Kama akina mama.

Tunaomba pia wenzetu wa bunge ambao hawako hapa tunahitaji watu wawe wanakuja kwa nyumba hii kwa sababu tumechaguliwa kuwakilisha wananchi ukiona Mheshimiwa Spika ni watu wachache sana huwa wanahudhuria katika nyumba hii si kila wakati watu wanakuja saa zile wanataka kwa hivyo mi naomba wakati ule mungu akitujalia tukirudi. Wakati huo mwingine watu wawe waje tufanye kazi yetu majukumu ambayo yametuleta hapa na tuweze kuwakilisha wale watu walio tuchagua, ahsante sana Bwana Spika na namshukuru mwenyezi mungu kwa muda huu.

**Specially Elected MCA,** (Hon. Osman Dube): Ahsante sana Bwana Spika, mimi leo nina furaha leo watu wanaongea Kiswahili na Mheshimiwa Asha anasema kuvunja nyumba ni kama Mheshimiwa tunaenda nyumbani. Ninaomba Mheshimiwa Asha sio kuvunja nyumba ni kufunga nyumba Bwana Spika (*ucheshi*) Nashukuru mimi kama Dube, nashukuru mwenyezi mungu nimekuwa miaka kadhaa hapa na mungu ametujalia siku hii ya leo tena.

Sisi kama bunge la Samburu kaunti umetushikilia sisi Bwana Spika tunaona tangu wewe kuingia jambo la ajabu mimi ninashangaa tangu uchaguliwe na sisi watu wa siasa wengine wanaenda hivi na wengine vile, sijui ulturoga au namna namna gani tukaenda mahali moja Bwana Spika.

Ninashukuru kazi hii tumeendesha na tuwe pamoja hata tukirudi tena mwezi wa pili mungu akitujalia tukirudi tushikilie jinsi saa hizi umetushikilia, ingawa huwezi kosa mmoja wetu mbaya au mzuri huwezi kosa Bwana Spika. Mimi ninashukuru na hii recess kubwa kwa kuanza sisi kama watu wa familia nyingi (*ucheshi*) inasaidia Bwana Spika kwa sababu tu naweza nenda kwa boma tofauti tofauti, tunashukuru Bwana Spika recess itakuwa sawa kwetu, ahsante sana Bwana Spika.

Bwana Spika ahsante kwa kunipatia nafasi tena kila kitu inakuwanga mnzuri kama kuna mapumziko kwa hivyo vile Mheshimiwa Asha amesema vile umesifiwa na waswahili wanasesma mgema akisifiwa tembo hilitia maji.

Kulingana na sheria ama sababu gani ilituleta hapa, kuna waheshimiwa wengine ni kama hawaji kabisa na nafikiri kama sijui sana ipo sharia wewe unayo ambayo umepewa na bunge hili.

Iwapo huna Mheshimiwa yejote ambaye ana shida mahali, hajaenda katika kamati, Bwana Spika ningependa tukianza mwaka tuanze na bidii kwa sababu kama tulikuja hapa tulikuja kuhudumia watu na kuna mambo mengine ambayo saa zingine ni aibu ukiona kwa mtandao hakuna akidi, na akidi ni watu tisa kamna hatufiki watu kumi hata?

Pia Mimi nawatakia kila mmoja wetu sikuu njema Krismasi, Mwaka mpya mungu atujalie atuweke vyema tukutane mwaka ujao lakini tuje na bidii ya kazi, kwamba tulikuja kwa hii nyumba kuhudumia watu na kaunti kwa jumla asante Bwana Spika.

**Specially Elected MCA,** (Lenolkulal Esther): Ahsante sana Bwana Spika ninashukuru kwa wakati huu na pia nashukuru mungu kwa sababu ametuwezesha tufike hapa. Kwa kweli, tangu

mimi nije hapa furaha yangu ilikuja tu wakati wewe ulikuja Bwana Spika, kwa sabbu wakati wa kwanza tulikuwa kama watoto ambao hawana mama au baba tunashindwa ni pande gani tuko hadi mimi nikawaambia wanangu hata mimi nataka kujiuzulu na kutoka huku kwa sababu afadhali kukaa kwangu ata na Amani kuliko kuja kuvunjika moyo kila siku. Kwa hivyo mimi nashukuru Mungu kwa sababu pengine ata Mungu alisikia maombi yetu kwamba hatukai vizuri. Kitu tu moja naomba waheshimiwa, tangu ukuje tumekuwa na Amani, pengine ata ndo maana watu hawakuji, kwa sababu wakati hiyo ya mbele, nafikiri kila mtu alikuwa anafika wa kwanza ata kabla ya madakika.

Kwa sababu tulikuwa tunapingana vibaya. Vile tulipata Amani watu wakatulia, kila mtu alienda kwake kufanya shughuli zake na pia si vizuri kwa sababu kuna watu bado tuliacha pale nyuma amabao wanatutegemea sisi na pia tuko kazi na si vizuri kwa sababu tunalipwa na ni dhambi kulipwa na haufiki kaz. Kwa hivyo ningeomba Mheshimiwa spika ujaribu tu kwa sababu sisi si watoto wa mama moja, kila mtu ametoka kwao na tabia yake. Kwa hivyo ni vizuri tu tujue tuko kazi hapa na wananchi wanatuongojapale nyumbani.

Utukaze tu kiazi Mheshimiowa Spika, usitulie sana kwa sababu watu watakuwa wakienda ata ukikaa tu pengine hauna shughuli kwa hivyo ningeomba tu tulishukuru Mungu na tuendelee vizuri, nawatakia kila la heri na tungangane, watu wetu wako na chida, iko mambo mengi ambayo tungestahili kujadiliana kwa hii nyumba.

Tuko na vitu mingi kwa sababu ata sahii sisi kama women coercers, tuko na policy mingi amabyo zimekaa mahali. Wamama hawasaidiki kwa hivyo naomba tu watu wakuje na mtuangalie pia kwa sababu siku ile tulikuwa huku, kwa vitu mingi sana sana ya wamama ambayo zimekaa hazijashughulikiwa kwa hivyo kwa msaada wako Mheshimiwa Spika, angalia ata upande ya wamama. Tunajua sahii kule mashinani, wamama ndo kila kitu, sai ata wale wako hapa, mtu anaenda kukaa kwa kitu kungojea chakula kile kilipikwa na kungonjea manguo iwoshwe, kwa hivyo tukirudi Mungu akituesesha, tunataka kuona tukisaidika kama wamama ndo tupate tuingie kwa sharia kama women coercers kwa hivyo naomba tusaidike kama wamama kabsa juu sasiingine tunakaliwa kiasi. Asante Mheshimiwa Spika.

**Specially Elected Member, (Hon. Lenamatiyo Silapia):** Thank you Hon. Speaker, thank you for giving me another chance to say something that have forgotten. I think the Hon. Member is

raising an issue of strengthening punctuality in this House. I think this House is very respected House in this County of Samburu and it is a must that we perform our duties as God has enable us to be here to represent, legislate and also to do an oversight but I know our God will enable us to come on February or even o January, I know in January we will usually have our committees, even December, we only close the House of the business but other businesses we will be having them.

It is my prayer and also the prayer of Hon. Members that as we go on to capture the women coercers as the committee within our standing order. It is our prayer. Just because when you see this House, each and every day and I want to give you a time, learn from this House. Who are those normally present in this House, they are normally nominated MCAs, there are normally women I this County Assembly so we want you to consider us, fight even if we are fighting for our space but we need your help.

Thank you Hon. Speaker. Hon. Members it is my prayer also that we will be in the function of the Speaker which will held in Nyiro Ward on Saturday God willing. Speaker we wish you well, we wish you a very protective and very peaceful your thanks giving. On my behalf and of my family, let me welcome you there even though I have ever been there, you are welcome to our Speakers Thanks giving. Thank you.

## **ADJOURNMENT**

**The Speaker, (Mr. Lenamarle Stephen):** Hon Members the time being seven minutes to four o'clock and there being no any other business, this Assembly now adjourns until Tuesday 13<sup>th</sup>, 2024 at 2:30 pm.